# Mhubiri

### *Kila kitu ni ubatili*

1 Maneno ya Mhubiri, mwana wa Daudi,
mfalme huko Yerusalemu:
2 “Ubatili! Ubatili!”
Mhubiri anasema.
“Ubatili mtupu!
Kila kitu ni ubatili.”

3 Mwanadamu anafaidi nini kutokana na kazi yake yote
anayotaabikia chini ya jua?
4 Vizazi huja na vizazi hupita,
lakini dunia inadumu milele.
5 Jua huchomoza na jua huzama,
nalo huharakisha kurudi mawioni.
6 Upepo huvuma kuelekea kusini
na kugeukia kaskazini;
hurudia mzunguko huo huo,
daima ukirudia njia yake.
7 Mito yote hutiririka baharini,
hata hivyo bahari kamwe haijai.
Mahali mito inapotoka,
huko hurudi tena.
8 Vitu vyote vinachosha,
kuliko mtu anavyoweza kusema.
Jicho kamwe halitosheki kutazama,
wala sikio halishibi kusikia.
9 Kile kilichokuwepo kitakuwepo tena,
kile kilichofanyika kitafanyika tena,
hakuna kilicho kipya chini ya jua.

10 Kuna kitu chochote ambacho mtu anaweza kusema,
“Tazama! Kitu hiki ni kipya”?
Kilikuwepo tangu zamani za kale,
kilikuwepo kabla ya wakati wetu.
11 Hakuna kumbukumbu ya watu wa zamani,
hata na wale ambao hawajaja bado
hawatakumbukwa
na wale watakaofuata baadaye.

### *Hekima ni ubatili*

12 Mimi, Mhubiri, nilikuwa mfalme wa Israeli
katika Yerusalemu.
13 Nilitumia muda wangu wote kujifunza na
kuvumbua kwa hekima yote yanayofanyika chini
ya mbingu. Jinsi gani Mungu ameweka mzigo
mzito juu ya wanadamu!
14 Nimeshaona mambo yote yanayotendeka
chini ya jua, hayo yote ni ubatili, hii ni kukimbiza
upepo.
15 Kilichopindika hakiwezi kunyooshwa;
kile ambacho hakipo haiwezekani kukihesabu.
16 Niliwaza mwenyewe, “Tazama, nimekua
na kuongezeka katika hekima kuliko yeyote
aliyewahi kutawala Yerusalemu kabla yangu.
Nimekuwa na uzoefu mkubwa wa hekima na
maarifa.”
17 Ndipo nilipojitahidi kufahamu kutofautisha
hekima, wazimu na upumbavu, lakini nikatambua
hata hili nalo ni kukimbiza upepo.
18 Kwa kuwa hekima nyingi huleta huzuni kubwa;
maarifa yanapoongezeka, masikitiko yanaongezeka.

# 2

*Anasa ni ubatili*

1 Nikafikiri moyoni mwangu, “Haya basi, ni-
takujaribu kwa anasa nione ni lipi lililo jema.”
Lakini hilo nalo likaonekana ni ubatili.
2 Nikasema, “Kicheko nacho ni upumbavu.
Nayo matokeo ya anasa ni nini?”
3 Nikajaribu kujifurahisha kwa mvinyo na
kukumbatia upumbavu, huku bado akili yangu
inaniongoza kwa hekima. Nilitaka kuona ni lipi
bora watu wafanye kwa siku chache wanazoishi
chini ya mbingu.

4 Nikafanya miradi mikubwa: Nikajijengea
majumba na kulima mashamba ya mizabibu.
5 Nikatengeneza bustani na viwanja vya
starehe; nikaotesha huko kila aina ya miti ya
matunda.
6 Nikajenga mabwawa ya kukusanya maji ya
kunyweshea hii miti iliyokuwa inastawi vizuri.
7 Nikanunua watumwa wa kiume na wa kike,
nao watumwa wengine walizaliwa nyumbani
mwangu. Pia nilikuwa na makundi ya ng’ombe,
kondoo na mbuzi kuliko mtu yeyote aliyewahi
kuishi Yerusalemu kabla yangu.
8 Nikajikusanyia fedha na dhahabu, hazina
za wafalme na za majimbo. Nikajipatia waim-
baji wanaume na wanawake, nazo nyumba za
masuria: vitu ambavyo moyo wa mwanadamu
hufurahia.
9 Nikawa maarufu sana kuliko mtu mwingine
yeyote aliyepata kuishi Yerusalemu kabla yangu.
Katika haya yote bado nikawa nina hekima.

10 Sikujinyima kitu chochote ambacho macho yangu yalikitamani,
hakuna anasa niliyounyima moyo wangu.
Moyo wangu ulifurahia kazi zangu zote,
hii ilikuwa thawabu ya kazi zangu zote.
11 Hata hivyo nilipokuja kuangalia yote ambayo mikono yangu ilikuwa imefanya
na yale niliyotaabika kukamilisha,
kila kitu kilikuwa ni ubatili, ni kukimbiza upepo;
hapakuwa na faida yoyote chini ya jua.

### *Hekima na upumbavu ni ubatili*

12 Kisha nikageuza mawazo yangu kufikiria hekima,
wazimu na upumbavu.
Ni nini zaidi mtu anayetawala baada ya mfalme
anachoweza kufanya ambacho hakijafanywa?
13 Nikaona kuwa hekima ni bora kuliko upumbavu,
kama vile nuru ilivyo bora kuliko giza.
14 Mtu mwenye hekima ana macho katika kichwa chake,
lakini mpumbavu anatembea gizani;
lakini nikaja kuona kwamba
wote wawili hatima yao inafanana.
15 Kisha nikafikiri moyoni mwangu,
“Hatima ya mpumbavu itanipata mimi pia.
Nitafaidi nini basi kwa kuwa na hekima?”
Nikasema moyoni mwangu,
“Hili nalo ni ubatili.”
16 Kwa maana kwa mtu mwenye hekima,
kama ilivyo kwa mpumbavu,
hatakumbukwa kwa muda mrefu,

katika siku zijazo wote watasahaulika.
Kama vile ilivyo kwa mpumbavu,
mtu mwenye hekima pia lazima atakufa!
17 Kwa hiyo nikachukia maisha, kwa sababu
kazi inayofanyika chini ya jua ilikuwa masikitiko
kwangu. Yote hayo ni ubatili, ni kukimbiza
upepo.

*Kutaabika ni ubatili*
18 Nikachukia kila kitu nilichokuwa
nimetaabikia chini ya jua, kwa sababu ni lazima
nimwachie yule ajaye baada yangu.
19 Nani ajuaye kama atakuwa ni mtu mwenye
hekima au mpumbavu? Lakini hata hivyo yeye
ndiye atakayetawala kazi zote ambazo nimemi-
minia juhudi na ustadi chini ya jua. Hili nalo ni
ubatili.
20 Kwa hiyo moyo wangu ukaanza kukata
tamaa juu ya kazi yangu yote niliyoifanya kwa
taabu chini ya jua.
21 Kwa kuwa mtu anaweza kufanya kazi yake
kwa hekima, maarifa na ustadi, kisha analaz-
imika kuacha vyote alivyo navyo kwa mtu
mwingine ambaye hajavifanyia kazi. Hili nalo
pia ni ubatili tena ni balaa kubwa.
22 Mtu atapata nini kwa taabu yote na
kuhangaika kwa bidii katika kazi anayotaabikia
chini ya jua?
23 Siku zake zote kazi yake ni maumivu na
masikitiko, hata usiku akili yake haipati ma-
pumziko. Hili nalo pia ni ubatili.
24 Hakuna kitu bora anachoweza kufanya mtu
zaidi ya kula na kunywa na kuridhika katika kazi

yake. Hili nalo pia, ninaona, latokana na mkono
wa Mungu,
25 kwa sababu pasipo yeye, ni nani awezaye
kula na kufurahi?
26 Kwa yule mtu anayempendeza Mungu,
Mungu humpa hekima, maarifa na furaha, bali
kwa mwenye dhambi Mungu humpa kazi ya
kukusanya na kuhifadhi utajiri ili Mungu ampe
yule anayempenda. Hili nalo pia ni ubatili, ni
kukimbiza upepo.

# 3

*Kila jambo lina wakati wake*

1 Kuna wakati kwa ajili ya kila jambo,
nayo majira kwa kila tendo chini ya mbingu:

2 wakati wa kuzaliwa na wakati wa kufa,
wakati wa kupanda na wakati wa kung'oa yaliyopandwa,
3 wakati wa kuua na wakati wa kuponya,
wakati wa kubomoa,
na wakati wa kujenga,
4 wakati wa kulia na wakati wa kucheka,
wakati wa kuomboleza na wakati wa kucheza,
5 wakati wa kutawanya mawe na wakati wa kukusanya mawe,
wakati wa kukumbatia na wakati wa kutokumbatia,
6 wakati wa kutafuta na wakati wa kupoteza,
wakati wa kuweka na wakati wa kutupa,
7 wakati wa kurarua na wakati wa kushona,

wakati wa kunyamaza na wakati wa kuzungumza,
8 wakati wa kupenda na wakati wa kuchukia,
wakati wa vita na wakati wa amani.
9 Mfanyakazi anapata faida gani kutokana na taabu yake?
10 Nimeona mzigo Mungu alioweka juu ya wanadamu.
11 Amefanya kila kitu kiwe kizuri kwa wakati wake. Pia ameiweka hiyo milele katika mioyo ya wanadamu, wala hawawezi kutambua kwa kina yale ambayo Mungu amefanya kuanzia mwanzo hadi mwisho.
12 Ninajua kwamba hakuna kitu bora kwa wanadamu kuliko kuwa na furaha na kutenda mema wakati wanapoishi.
13 Tena ni karama ya Mungu kila mtu apate kula na kunywa na kujiburudisha kwa mema katika kazi yake yote.
14 Ninajua kwamba kila kitu anachokifanya Mungu kitadumu milele, hakuna kinachoweza kuongezwa au kupunguzwa. Mungu hufanya hivyo ili watu wamche yeye.
15 Chochote kilichopo kilishakuwepo,
na kitakachokuwepo kimekwishakuwepo;
naye Mungu huyaita yale yaliyopita yarudi tena.
16 Pia nikaona kitu kingine tena chini ya jua:
Mahali pa kutolea hukumu,
uovu ulikuwepo,
mahali pa kupatia haki,
uovu ulikuwepo.
17 Nikafikiri moyoni mwangu,
“Mungu atawaleta hukumuni

wote wawili wenye haki na waovu,
kwa maana kutakuwako na wakati kwa ajili ya kila jambo,
wakati kwa ajili ya kila tendo."
18 Pia nikafikiri, "Kuhusu wanadamu, Mungu
huwajaribu ili wajione kwamba wao ni kama
wanyama.
19 Hatima ya mwanadamu ni kama ile ya
wanyama; wote wana mwisho unaofanana:
Jinsi anavyokufa mnyama, ndivyo anavyokufa
mwanadamu. Wote wana pumzi inayofanana;
mwanadamu hana cha kumzidi mnyama. Kila
kitu ni ubatili.
20 Wote huenda mahali panapofanana; wote
hutoka mavumbini, mavumbini wote hurudi.
21 Ni nani ajuaye kama roho ya mtu huenda juu
na roho ya mnyama hushuka chini ardhini?"
22 Kwa hiyo nikaona kwamba hakuna kitu
kilicho bora zaidi kwa mwanadamu kuliko kuifurahia kazi yake, kwa sababu hilo ndilo fungu lake. Kwa maana ni nani awezaye kumrudisha ili aje kuona kile kitakachotendeka baada yake?

# 4

*Uonevu, taabu, uadui*

1 Nikatazama tena nikaona uonevu wote
uliokuwa unafanyika chini ya jua:
Nikaona machozi ya waliodhulumiwa,
wala hawana mfariji;
uwezo ulikuwa upande wa wale wanaowadhulumu,
lakini hawakuwa na mfariji.
2 Nami nikasema kwamba wafu,

waliokwisha kufa,
wana furaha kuliko watu walio hai,
ambao bado wanaishi.
3 Lakini aliye bora kuliko hao wawili
ni yule ambaye hajazaliwa bado,
ambaye hajaona ule uovu
unaofanyika chini ya jua.
4 Tena nikaona kuwa kazi zote na mafanikio
yote huchipuka kutokana na wivu wa mtu kwa
jirani yake. Hili nalo ni ubatili, ni kukimbiza
upepo.
5 Mpumbavu hukunja mikono yake
na kujiangamiza mwenyewe.
6 Afadhali konzi moja pamoja
na utulivu kuliko konzi mbili pamoja na taabu
na kukimbiza upepo.
7 Tena nikaona kitu kingine kilicho ubatili chini
ya jua:
8 Kulikuwa na mtu aliye peke yake,
hakuwa na mwana wala ndugu.
Hapakuwa na mwisho wa kazi yake;
hata hivyo macho yake
hayakutosheka na utajiri wake.
Aliuliza, "Ninajitaabisha hivi kwa ajili ya nani,
nami kwa nini ninajinyima kufurahia?"
Hili pia ni ubatili,
ni shughuli yenye taabu!

9 Wawili ni afadhali kuliko mmoja,
kwa sababu wana malipo mazuri kwa kazi yao:
10 Kama mmoja akianguka,
mwenzake atamwinua.

Lakini ni jambo la kuhuzunisha
kwa mtu yule aangukaye
naye hana wa kumwinua!
11 Pia, kama wawili wakilala pamoja
watapashana joto.
Lakini ni vipi mtu aweza
kujipasha joto mwenyewe?
12 Ingawa mtu mmoja aweza kushindwa,
watu wawili wanaweza
kumkabili adui na kumshinda.
Kamba ya nyuzi tatu
haikatiki kwa urahisi.

### *Maendeleo ni ubatili*

13 Afadhali kijana maskini mwenye hekima
kuliko mfalme mzee mpumbavu ambaye hajui
tena kupokea maonyo.
14 Kijana huyo angeweza kutokea gerezani
akapata ufalme, au angeweza kuwa amezaliwa
katika umaskini kwenye huo ufalme.
15 Nikaona kwamba wote walioishi na kutem-
bea chini ya jua walimfuata kijana, aliyepokea
ufalme.
16 Hapakuwa na kikomo cha watu wote
aliowatawala. Lakini wale waliokuja baadaye
hawakufurahia kazi ya yule aliyepokea ufalme.
Hili nalo pia ni ubatili, ni kukimbiza upepo.

# 5

### *Mche Mwenyezi Mungu*

1 Linda hatua zako uendapo katika nyumba
ya Mungu. Karibia usikilize kuliko kutoa
dhabihu ya wapumbavu, ambao hawajui kuwa
wanafanya kosa.

2 Usiwe mwepesi kuzungumza,
usiwe na haraka katika moyo wako
kuzungumza lolote mbele za Mungu.
Mungu yuko mbinguni
nawe uko duniani,
kwa hiyo maneno yako
na yawe machache.
3 Kama vile ndoto huja
wakati kuna shughuli nyingi,
ndivyo yalivyo mazungumzo ya mpumbavu
wakati kuna maneno mengi.
4 Unapomwekea Mungu nadhiri, usikawie
kuitimiza. Yeye hafurahii wapumbavu; timiza
nadhiri yako.
5 Ni afadhali usiweke nadhiri kuliko kuiweka
na usiitimize.
6 Usiruhusu kinywa chako kukuingiza dham-
bini. Tena usijitetee mbele ya huyo mjumbe
wa hekaluni, ukisema, “Niliweka nadhiri kwa
makosa.” Kwa nini Mungu akasirike kwa ajili
ya yale unayosema na kuiharibu kazi ya mikono
yako?
7 Kuota ndoto kwingi na maneno mengi ni
ubatili. Kwa hiyo mche Mungu.

### *Utajiri ni ubatili*

8 Ukiona maskini wanaodhulumiwa katika
nchi, na hukumu na haki vikipotoshwa, usis-
hangazwe na mambo hayo; kwa maana afisa
mmoja anaangaliwa na aliye juu yake, na juu ya
hao wawili kuna wengine walio juu yao.
9 Mafanikio ya nchi ni kwa ajili ya wote, hata
mfalme mwenyewe hufaidi kutoka mashambani.
10 Yeyote apendaye fedha kamwe

hatosheki na fedha;
yeyote apendaye utajiri kamwe
hatosheki na kipato chake.
Hili nalo pia ni ubatili.

11 Mali ikiongezeka, ndivyo walaji
wanavyoongezeka.
Hii nayo inamfaidia nini mwenye mali
isipokuwa ni kushibisha macho yake?

12 Usingizi wa kibarua ni mtamu,
awe amekula kidogo au kingi,
lakini wingi wa mali
humnyima tajiri usingizi.
13 Nimeshaona uovu mzito chini ya jua:
Utajiri uliolimbikizwa
na kuleta madhara kwa mwenye mali;
14 au utajiri uliopotea kwa bahati mbaya,
kiasi kwamba wakati akiwa na mwana
hakuna chochote kilichobaki kwa ajili yake.
15 Mtu hutoka tumboni mwa mama yake uchi,
naye jinsi alivyokuja vivyo hivyo huondoka.
Hachukui chochote kutokana na kazi yake
ambacho anaweza kukibeba mkononi
mwake.
16 Hili nalo ni baya la kusikitisha:
Kama vile mtu ajavyo, vivyo hivyo huondoka,
naye anapata faida gani,
maadamu hutaabika kwa ajili ya upepo?
17 Siku zake zote hula gizani,
pamoja na fadhaa kubwa,
mateso na hasira.

18 Ndipo nikatambua kwamba ni vyema na
sahihi kwa mtu kula na kunywa na kutosheka
katika kazi yake ngumu chini ya jua katika siku
chache za maisha yake Mungu alizompa, kwa
maana hili ndilo fungu lake.
19 Zaidi ya yote, Mungu anapompa mtu yey-
ote utajiri na milki, humwezesha kuvifurahia,
kukubali fungu lake na kuwa na furaha katika
kazi yake, hii ni karama ya Mungu.
20 Mara chache mtu huzifikiri siku za maisha
yake, kwa sababu Mungu humfanya ashikwe na
furaha ya moyoni.

# 6

1 Nimeona ubaya mwingine chini ya jua, nao
unalemea sana wanadamu:
2 Mungu humpa mwanadamu utajiri, mali na
heshima, hivyo hakukosa chochote moyo wake
unachokitamani. Lakini Mungu hamwezeshi
kuvifurahia, badala yake mgeni ndiye anayevifu-
rahia. Hili ni ubatili, ni ubaya unaosikitisha.

3 Mtu anaweza kuwa na watoto mia moja
naye akaishi miaka mingi, lakini haidhuru kuwa
ataishi muda mrefu kiasi gani, kama hawezi
kufurahia mafanikio yake na kwamba hapati
mazishi ya heshima, ninasema afadhali mtoto
aliyezaliwa akiwa amekufa kuliko yeye.
4 Kuzaliwa kwake hakuna maana, huondokea
gizani na gizani jina lake hufunikwa.
5 Ingawa hakuwahi kuliona jua wala kujua kitu
chochote, yeye ana pumziko kuliko mtu huyo:

6 Hata kama huyo mtu ataishi miaka elfu
mara mbili na zaidi, lakini akashindwa kufu-
rahia mafanikio yake, je, wote hawaendi sehemu
moja?
7 Juhudi zote za binadamu ni kwa ajili ya kinywa
chake,
hata hivyo hamu yake kamwe haitoshelezwi.
8 Mtu mwenye hekima ana faida gani
zaidi ya mpumbavu?
Mtu maskini anapata faida gani
kwa kujua jinsi ya kujistahi
mbele ya watu wengine?
9 Ni bora kile ambacho jicho linakiona
kuliko hamu isiyotoshelezwa.
Hili nalo ni ubatili,
ni kukimbiza upepo.

10 Lolote lililopo limekwisha kupewa jina,
naye mwanadamu alivyo ameshajulikana;
hakuna mtu awezaye kushindana
na mwenye nguvu kuliko yeye.
11 Maneno yanavyokuwa mengi,
ndivyo yanavyokosa maana,
Je, hilo linamfaidia vipi yeyote?
12 Kwa maana ni nani anayejua lililo jema
kwa ajili ya maisha ya mwanadamu, katika siku
chache na za ubatili anazopita kama kivuli? Ni
nani awezaye kumwambia yatakayotokea chini
ya jua baada ya yeye kuondoka?

# 7

*Hekima*

1 Afadhali sifa nzuri kuliko manukato safi,

nayo siku ya kufa kuliko ya kuzaliwa.
2 Afadhali kwenda kwenye nyumba ya msiba
kuliko kwenda kwenye nyumba ya karamu,
kwa kuwa kifo ni hatima ya kila mwanadamu,
imewapasa walio hai kuliweka hili mioyoni mwao.
3 Huzuni ni afadhali kuliko kicheko,
kwa sababu uso wenye huzuni wafaa kwa moyo.
4 Moyo wa wenye hekima uko katika nyumba ya msiba,
lakini moyo wa wapumbavu uko katika nyumba ya anasa.
5 Afadhali kusikia karipio la mtu mwenye hekima,
kuliko kusikiliza wimbo wa wapumbavu.
6 Kama ilivyo kuvunjika kwa miiba chini ya sufuria,
ndivyo kilivyo kicheko cha wapumbavu.
Hili nalo pia ni ubatili.

7 Dhuluma humfanya mtu mwenye hekima kuwa mpumbavu,
nayo rushwa huuharibu moyo.

8 Mwisho wa jambo ni bora kuliko mwanzo wake,
uvumilivu ni bora kuliko kiburi.
9 Usiwe mwepesi kukasirika rohoni mwako,
kwa kuwa hasira hukaa kifuani mwa wapumbavu.

10 Usiseme, “Kwa nini siku za kale
zilikuwa bora kuliko siku hizi?”
Kwa maana si hekima

kuuliza maswali kama hayo.

11 Hekima, kama ulivyo urithi, ni kitu chema
na huwafaidia wale walionalo jua.
12 Hekima ni ulinzi
kama fedha ilivyo ulinzi,
lakini faida ya maarifa ni hii:
kwamba hekima huhifadhi maisha ya aliye nayo.
13 Tafakari kile Mungu alichokitenda:
Nani awezaye kunyoosha
kile ambacho yeye amekipinda?
14 Nyakati zikiwa nzuri, ufurahi,
lakini nyakati zikiwa mbaya, tafakari hili:
Mungu amefanya hiyo moja;
naam, pia na hiyo nyingine.
Kwa hiyo, mwanadamu hawezi kugundua
kitu chochote kuhusu maisha yake ya baadaye.
15 Katika maisha haya yangu ya ubatili nime-
shaona haya mawili:
mtu mwadilifu akiangamia katika uadilifu wake,
naye mtu mwovu akiishi maisha marefu katika uovu wake.
16 Usiwe mwenye haki kupita kiasi,
wala usiwe na hekima kupita kiasi:
kwa nini kujiangamiza mwenyewe?
17 Usiwe mwovu kupita kiasi,
wala usiwe mpumbavu:
kwa nini kufa kabla ya wakati wako?
18 Ni vyema kushika hilo moja
na wala usiache hilo jingine likupite.

Mtu amchaye Mungu ataepuka huko kupita
kiasi.*

19 Hekima humfanya yeye aliye nayo kuwa na
uwezo
kuliko watawala kumi katika mji.

20 Hakuna mtu mwenye haki duniani
ambaye hufanya mambo ya haki
na kamwe asitende dhambi.

21 Usitie maanani kila neno linalosemwa na watu,
la sivyo, unaweza kumsikia
mtumishi wako akikulaani:
22 kwa kuwa unafahamu moyoni mwako
kwamba wewe mwenyewe mara nyingi
umewalaani wengine.
23 Yote haya niliyajaribu kwa hekima,
nikasema,
“Nimeamua kuwa na hekima”:
lakini hii ilikuwa nje ya uwezo wangu.
24 Vyovyote hekima ilivyo,
hekima iko mbali sana na imejificha,
ni nani awezaye kuigundua?
25 Nikageuza fikira zangu ili kuelewa,
kuchunguza na kuitafuta hekima
na kusudi la mambo,
na ili kuelewa ujinga wa uovu,
na wazimu wa upumbavu.

26 Nimeona jambo lililo chungu kuliko mauti,
mwanamke ambaye ni mtego,

---

* **7:18** au *Mtu amchaye Mwenyezi Mungu atafuata hayo yote mawili.*

ambaye moyo wake ni wavu wa kutegea
na mikono yake ni minyororo.
Mtu ampendezaye Mungu atamkwepa,
bali mwenye dhambi atanaswa naye.
27 Mhubiri anasema, "Tazama, hili ndilo nililo-
gundua:
"Nimegundua kitu kimoja baada ya kingine
nilipokuwa katika kusudi la mambo:
28 ningali natafiti
lakini sipati:
nilimpata mwanaume mmoja mnyofu miongoni
mwa elfu,
lakini hakuna mwanamke mmoja mnyofu
miongoni mwao.
29 Hili ndilo peke yake nililolipata:
Mungu amemuumba mwanadamu mnyofu,
lakini mwanadamu amebuni mambo
mengi."

# 8

1 Ni nani aliye kama mtu mwenye hekima?
Ni nani ajuaye maelezo ya mambo?
Hekima hung'arisha uso wa mtu na kubadili
ugumu wa uso wake.

## *Mtii mfalme*

2 Nawaambia, Tii amri ya mfalme, kwa sababu
uliapa mbele za Mungu.
3 Usiharakishe kuondoka mbele ya mfalme.
Usiendelee kutenda lililo baya, kwa maana
mfalme atafanya lolote apendalo.

4 Kwa kuwa neno la mfalme ndilo lenye mam-
laka ya mwisho, nani awezaye kumwambia, “Je,
wewe unafanya nini?”

5 Yeyote anayetii agizo lake hatadhurika,
moyo wa hekima utajua wakati mwafaka
na jinsi ya kutenda.
6 Kwa maana kuna wakati mwafaka
na utaratibu wa kila jambo,
ingawa huzuni ya mwanadamu
huwa nzito juu yake.
7 Kwa vile hakuna mtu ajuaye siku zijazo,
ni nani awezaye kumwambia linalokuja?
8 Hakuna mwanadamu
awezaye kushikilia roho yake asife,
wala hakuna mwenye uwezo
juu ya siku ya kufa kwake.
Kama vile hakuna yeyote arudishwaye nyuma
wakati wa vita,
kadhalika uovu hautawaweka huru wale
wautendao.

9 Yote haya niliyaona, nilipokuwa natafakari
kila kitu kinachotendeka chini ya jua. Kuna
wakati mtu hujifanya bwana juu ya wengine kwa
madhara yake mwenyewe.

10 Ndipo pia nikaona waovu wakizikwa, wale
waliozoea kuingia na kutoka mahali patakatifu
na kupewa sifa katika mji ambao waliyafanya
haya. Hili nalo ni ubatili.

11 Wakati hukumu juu ya tendo ovu
haitekelezwi upesi, mioyo ya watu hujaa
mipango ya kutenda maovu.

12 Ingawa mtu mwovu hufanya maovu mia
moja na akaendelea kuishi maisha marefu, najua

kwamba itakuwa bora zaidi kwa watu wanaomwogopa Mungu, wamchao Mungu.
13 Lakini kwa sababu waovu hawamwogopi
Mungu, hawatafanikiwa, maisha yao hayatarefuka kama kivuli.
14 Kuna kitu kingine ambacho ni ubatili kinachofanyika duniani: Watu waadilifu kupata yale yanayowastahili waovu, nao waovu kupata yale yanayowastahili waadilifu. Hili nalo pia, nasema ni ubatili.
15 Kwa hiyo mimi ninasifu kufurahia maisha,
kwa sababu hakuna kitu bora zaidi kwa mwanadamu chini ya jua kuliko kula, kunywa na kufurahi. Kisha furaha itafuatana naye kazini mwake siku zote za maisha yake ambazo amepewa na Mungu chini ya jua.
16 Nilipotafakari akilini mwangu ili nijue
hekima na kuangalia kazi ya mwanadamu duniani, jinsi macho yake hayapati usingizi mchana wala usiku,
17 ndipo nikaona yale yote ambayo Mungu
ameyafanya. Hakuna yeyote awezaye kuelewa yale yanayotendeka chini ya jua. Licha ya juhudi zake zote za kutafuta, mtu hawezi kugundua maana yake. Hata ingawa mtu mwenye hekima anadai kuwa anafahamu, kwa hakika hawezi kutambua.

# 9

*Hatima ya wote*

1 Kwa hiyo niliyatafakari haya yote, nikafikia
uamuzi kwamba waadilifu na wenye hekima na yale wanayoyafanya yako mikononi mwa

Mungu, lakini hakuna mtu ajuaye kama anangojewa na upendo au chuki.

2 Wote wanayo hatima inayofanana, mwadilifu
na mwovu, mwema na mbaya, aliye safi na aliye
najisi, wale wanaotoa dhabihu na wale wasiotoa.
Kama ilivyo kwa mtu mwema,
ndivyo ilivyo kwa mtu mwenye dhambi;
kama ilivyo kwa wale wanaoapa,
ndivyo ilivyo kwa wale wasioapa.

3 Huu ni ubaya ulio katika kila kitu kinachotendeka
chini ya jua: Mwisho unaofanana huwapata
wote. Zaidi ya hayo, mioyo ya watu, imejaa
ubaya na kuna wazimu mioyoni mwao wangali
hai, hatimaye huungana na waliokufa.

4 Yeyote aliye miongoni mwa walio hai analo
tumaini, hata mbwa hai ni bora kuliko simba
aliyekufa!

5 Kwa maana walio hai wanajua kwamba watakufa,
lakini wafu hawajui chochote,
hawana tuzo zaidi,
hata kumbukumbu yao imesahaulika.

6 Upendo wao, chuki yao na wivu wao
vimetoweka tangu kitambo,
kamwe hawatakuwa tena na sehemu
katika lolote linalotendeka chini ya jua.

7 Nenda, kula chakula chako kwa furaha, unywe
divai yako kwa moyo wa shangwe, kwa
maana sasa Mungu anakubali unachofanya.

8 Daima uvae nguo nyeupe na daima upake
kichwa chako mafuta.

9 Furahia maisha na mke wako, umpendaye,
siku zote za maisha ya ubatili uliyopewa na

Mungu chini ya jua, siku zote za ubatili. Kwa maana hili ndilo fungu lako katika maisha na katika kazi yako ya taabu chini ya jua.

10 Lolote mkono wako upatalo kufanya, fanya kwa nguvu zako zote, kwa kuwa huko Kuzimu*, unakoenda, hakuna kufanya kazi wala mipango wala maarifa wala hekima.

11 Nimeona kitu kingine tena chini ya jua:
Si wenye mbio washindao mashindano
au wenye nguvu washindao vita,
wala si wenye hekima wapatao chakula
au wenye akili nyingi wapatao mali,
wala wenye elimu wapatao upendeleo,
lakini fursa huwapata wote.

12 Zaidi ya hayo, hakuna mwanadamu ajuaye wakati saa yake itakapokuja:
Kama vile samaki wavuliwavyo katika wavu mkatili,
au ndege wanaswavyo kwenye mtego,
vivyo hivyo wanadamu hunaswa na nyakati mbaya
zinazowaangukia bila kutazamia.

### *Hekima ni bora kuliko upumbavu*

13 Pia niliona chini ya jua mfano huu wa hekima ambao ulinivutia sana:
14 Palikuwa na mji mdogo uliokuwa na watu wachache ndani yake. Mfalme mwenye nguvu akainuka dhidi yake, akauzingira kwa jeshi kubwa.

* **9:10** Kuzimu kwa Kiebrania ni *Sheol*, yaani *Shimo lisilo na mwisho.*

15 Katika mji huo kulikuwa na mtu mmoja
maskini lakini mwenye hekima, naye akauokoa
ule mji kwa hekima yake. Lakini hakuna
aliyemkumbuka yule maskini.
16 Kwa hiyo, nikasema, "Hekima ni bora ku-
liko nguvu." Lakini hekima ya maskini imed-
harauliwa, wala hakuna anayesikiliza maneno
yake.
17 Maneno ya utulivu ya mwenye hekima
husikiwa kuliko makelele ya mtawala wa wapumbavu.
18 Hekima ni bora kuliko silaha za vita,
lakini mwenye dhambi mmoja
huharibu mema mengi.

# 10

1 Kama vile inzi waliokufa huacha harufu mbaya kwenye manukato,
ndivyo upumbavu kidogo huzidi nguvu hekima na heshima.
2 Moyo wa mwenye hekima huelekea kuume,
lakini moyo wa mpumbavu huelekea kushoto.
3 Hata anapotembea barabarani,
mpumbavu hukosa ufahamu
na kudhihirisha kwa kila mmoja
jinsi alivyo mpumbavu.
4 Kama hasira ya mtawala ikiwaka dhidi yako,
usiache mahali pako,
utulivu huweza kuzuia makosa mengi.

5 Kuna ubaya niliouona chini ya jua,

aina ya kosa litokalo kwa mtawala:
6 Wapumbavu kuwekwa kwenye nafasi nyingi za utawala,
hali matajiri wanashika nafasi za chini.
7 Mimi nimeona watumwa wamepanda farasi,
wakati wakuu wakitembea
kwa miguu kama watumwa.

8 Yeye achimbaye shimo
aweza kutumbukia ndani yake,
yeyote abomoaye ukuta
anaweza kuumwa na nyoka.
9 Yeyote apasuaye mawe
inawezekana yakamuumiza,
yeyote apasuaye magogo
inawezekana yakamuumiza.

10 Kama shoka ni butu
na halikunolewa,
nguvu nyingi zinahitajika,
lakini ustadi utaleta mafanikio.

11 Nyoka akiuma kabla ya kuchezeshwa,
mchezeshaji hatahitajika tena.

12 Maneno yanayotoka kinywani mwa mtu mwenye hekima yana neema,
bali mpumbavu huangamizwa
na midomo yake mwenyewe.
13 Mwanzoni maneno yake ni upumbavu,
mwishoni ni wazimu mbaya,
14 naye mpumbavu huzidisha maneno.

Hakuna yeyote ajuaye linalokuja,
ni nani awezaye kueleza ni jambo gani
litakalotokea baada yake?

15 Kazi ya mpumbavu humchosha mwenyewe,
hajui njia iendayo mjini.

16 Ole wako, ee nchi ambayo mfalme wako alikuwa mtumwa
na ambayo wakuu wako hufanya karamu asubuhi.
17 Heri wewe, ee nchi ambayo mfalme wako
ni wa uzao wenye kuheshimika,
na ambayo wakuu wako hula chakula
kwa wakati unaofaa:
wao hula ili kupata nguvu
na si kwa ajili ya ulevi.

18 Kama mtu ni mvivu, paa la nyumba huinama;
kutokana na mikono milegevu, nyumba huvuja.

19 Karamu hufanywa kwa ajili ya kicheko,
nao mvinyo hufurahisha maisha,
lakini fedha ni jawabu la mambo yote.

20 Usimshutumu mfalme hata ikiwa ni katika mawazo yako,
au kumlaani tajiri katika chumba chako cha kulala,
kwa sababu ndege wa angani wanaweza kuchukua maneno yako,

naye ndege anayeruka anaweza kutoa taar-
ifa ya yale uliyosema.

# 11

### *Mkate juu ya maji*

1 Tupa mkate wako juu ya maji,
kwa maana baada ya siku nyingi
utaupata tena.
2 Wape sehemu watu saba, naam hata wanane,
kwa maana hujui ni baa gani
litakalokuwa juu ya nchi.

3 Kama mawingu yamejaa maji,
hunyesha mvua juu ya nchi.
Kama mti ukianguka kuelekea kusini
au kuelekea kaskazini,
mahali ulipoangukia,
hapo ndipo utakapolala.
4 Yeyote atazamaye upepo hatapanda,
yeyote anayeangalia mawingu hatavuna.

5 Kama vile usivyofahamu njia ya upepo,
au jinsi mwili uumbwavyo
ndani ya tumbo la mama,
vivyo hivyo huwezi kufahamu kazi ya Mungu,
Muumba wa vitu vyote.

6 Panda mbegu yako asubuhi,
nako jioni usiruhusu mikono yako ilegee,
kwa maana hujui ni ipi itakayofanikiwa,
kwamba ni hii au ni ile,
au kwamba zote zitafanikiwa sawasawa.

### *Mkumbuke Muumba wako ukiwa bado kijana*

7 Nuru ni tamu,
tena inafurahisha macho kuona jua.
8 Mtu akiishi miaka mingi kiasi gani,
na aifurahie yote.
Lakini akumbuke siku za giza,
kwa maana zitakuwa nyingi.
Kila kitu kitakachokuja ni ubatili.

9 Furahi ewe kijana, ukiwa bado kijana,
moyo wako na ukupe furaha
siku za ujana wako.
Fuata njia za moyo wako
na chochote macho yako yanaona,
lakini ujue kwamba kwa ajili ya haya yote
Mungu atakuleta hukumuni.
10 Kwa hiyo, ondoa wasiwasi moyoni mwako
na utupilie mbali masumbufu ya mwili wako,
kwa kuwa ujana na nguvu ni ubatili.

## 12

1 Mkumbuke Muumba wako
siku za ujana wako,
kabla hazijaja siku za taabu,
wala haijakaribia miaka utakaposema,
"Mimi sifurahii hiyo":
2 kabla jua na nuru,
nao mwezi na nyota havijatiwa giza,
kabla ya kurudi mawingu baada ya mvua;
3 siku ile walinzi wa nyumba watakapotetemeka,
nao watu wenye nguvu watakapojiinamisha,

wakati wasagao watakapokoma kwa sababu ya uchache,
nao wachunguliao madirishani kutiwa giza;
4 wakati milango ya kuingia barabarani itakapofungwa
na sauti ya kusaga kufifia;
wakati watu wataamshwa kwa sauti ya ndege,
lakini nyimbo zao zote zikififia;
5 wakati watu watakapoogopa kilichoinuka juu
na hatari zitakazokuwepo barabarani;
wakati mlozi utakapochanua maua
na panzi kujikokota
nawe usiwe na shauku ya kitu chochote.
Ndipo mwanadamu aiendea nyumba yake ya milele
nao waombolezaji wakizunguka barabarani.

6 Mkumbuke Muumba wako: kabla haijakatika kamba ya fedha,
au bakuli la dhahabu halijavunjika;
kabla mtungi kuvunjika kwenye chemchemi,
au gurudumu kuvunjika kisimani,
7 nayo mavumbi kurudi ardhini yalikotoka,
na roho kurudi kwa Mungu aliyeitoa.

8 Mhubiri asema, “Ubatili! Ubatili!
Kila kitu ni ubatili!”

### *Hitimisho la mambo yote*

9 Mhubiri hakuwa tu na hekima, bali aliwagawia watu maarifa pia. Alitafakari na kutafiti na akaweka katika utaratibu mithali nyingi.
10 Mhubiri alitafiti ili kupata maneno sahihi na kila alichoandika kilikuwa sawa na kweli.

11 Maneno ya wenye hekima ni kama
mchokoro, mithali zao zilizokusanywa pamoja
ni kama misumari iliyopigiliwa ikawa imara,
yaliyotolewa na Mchungaji mmoja.
12 Zaidi ya hayo, mwanangu, kubali maonyo.

Hakuna mwisho wa kutunga vitabu vingi, nako kusoma sana huuchosha mwili.

13 Hii ndiyo jumla ya maneno;
yote yamekwisha sikiwa:
Mche Mungu, nawe uzishike amri zake,
maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu.
14 Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi,
pamoja na kila neno la siri,
likiwa jema au baya.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible."

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

- If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.
- If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d